**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA**

# TAARIFA YA HALI YA DAWA ZA KULEVYA YA MWAKA 2020

**Imetayarishwa kwa mujibu wa Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (Sura 95)**

**Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya ya Mwaka 2020**

**Imetayarishwa na**
**Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya,**
**S.L.P 80327,**
**8 Barabara ya Kivukoni,**
**11486 Dar es Salaam**
**Barua pepe:cg@dcea.go.tz**
**Tovuti: www.dcea.go.tz**
**Instagram: @dceatanzania**
**Twitter: @dceatanzania**
**Facebook: dcea_tz**
**YouTube:DCEATV**

**ISBN:978-9987-9596-9-3**

**Imetayarishwa kwa mujibu wa Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (Sura 95)**

## YALIYOMO

**YALIYOMO** ........................................................................................ ii
**ORODHA YA MAJEDWALI** .......................................................................... iv
**ORODHA YA VIELELEZO** ........................................................................... v
**MAELEZO YA WAZIRI** ............................................................................... vii
**DIBAJI** ....................................................................................................... viii
**FAHARASA** ................................................................................................ ix
**SURA YA KWANZA** ...................................................................................... 1
**TATIZO LA DAWA ZA KULEVYA DUNIANI** .................................................... 1
1.1 Utangulizi ................................................................................................... 1
1.2 Matumizi ya Dawa za Kulevya ...................................................................... 1
1.3 Biashara ya Dawa za Kulevya Duniani ......................................................... 2
1.4 Matibabu kwa Waraibu wa Dawa za Kulevya ................................................. 5
1.5 Changamoto za Udhibiti wa Tatizo la Dawa za Kulevya ................................. 6
1.6 Janga la Virusi vya Corona (COVID-19) ........................................................ 7
1.6.1 Uzalishaji wa Dawa za Kulevya ................................................................. 7
1.6.2 Usafirishaji wa Dawa za Kulevya ............................................................... 9
1.6.3 Matumizi ya Dawa za Kulevya .................................................................. 11
**SURA YA PILI** ............................................................................................. 13
**MIKAKATI YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA NCHINI...** .13
2.1 Utangulizi ................................................................................................... 13
2.2 Kudhibiti Upatikanaji wa Dawa za Kulevya (Supply Reduction) ....................... 13
2.3 Kupunguza Uhitaji wa Dawa za Kulevya (Demand Reduction) ......................... 13
2.4 Kupunguza Madhara ya Matumizi ya Dawa za Kulevya (Harm Reduction) 13
2.5 Kuimarisha Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa .......................................... 14
**SURA YA TATU** ........................................................................................... 15
**KUDHIBITI UPATIKANAJI WA DAWA ZA KULEVYA** ...................................... 15
3.1 Utangulizi ................................................................................................... 15
3.2 Kudhibiti Upatikanaji wa Dawa za Kulevya .................................................... 15
3.3 Uchunguzi wa Kimaabara wa Dawa za Kulevya ............................................ 22

3.4 Udhibiti wa Kemikali Bashirifu ........................................................................23

3.5 Udhibiti wa Dawa Tiba Zenye Asili ya Kulevya..........................................24

3.6 Ushirikiano Katika Udhibiti wa Kemikali Bashirifu na Dawa Tiba Zenye Asili ya Kulevya.......................................................................................25

3.7 Uteketezaji wa Dawa za Kulevya ..............................................................25

**SURA YA NNE.............................................................................................27**

**KUPUNGUZA UHITAJI WA DAWA ZA KULEVYA ......................................27**

4.1 Utangulizi........................................................................................................27

4.2 Matumizi ya Dawa za Kulevya Nchini.........................................................27

4.3 Sababu Zinazochangia Matumizi ya Dawa za Kulevya.............................27

4.4 Madhara ya Dawa za Kulevya.......................................................................28

4.5 Jitihada Zilizofanyika Katika Kupunguza Uhitaji .........................................31

4.5.1 Uelimishaji Uliofanywa na Mamlaka..................................................31

4.5.2 Uelimishaji uliofanywa na Wadau .....................................................32

**SURA YA TANO ............................................................................................34**

**KUPUNGUZA MADHARA YA MATUMIZI YA DAWA ZA KULEVYA ...........34**

5.1 Utangulizi........................................................................................................34

5.2 Huduma za Upunguzaji Madhara kwa Waraibu ........................................34

5.2.1 Tiba ya Uraibu wa Dawa za Kulevya Katika Vitengo vya Afya ya Akili Nchini.......................................................................................34

5.2.2 Huduma ya Upataji Nafuu kwenye Asasi za Kiraia .............................35

5.2.3 Huduma ya Tiba Dawa.........................................................................36

5.2.4 Nyumba za Upataji Nafuu (Sober Houses) ........................................41

5.3 Faida za Huduma za Upunguzaji madhara kwa Waraibu .........................43

**SURA YA SITA .............................................................................................45**

**CHANGAMOTO NA HATUA ZA BAADAYE .................................................45**

6.1 Utangulizi........................................................................................................45

6.2 Changamoto ...................................................................................................45

6.3 Hatua za Baadaye ..........................................................................................45

## ORODHA YA MAJEDWALI

**Jedwali Na. 1:** Kiasi cha Bangi na Mirungi Kilichokamatwa Nchini Kati ya Mwaka 2011-2020……………………………………………16

**Jedwali Na. 2**: Idadi ya Watuhumiwa wa Bangi na Mirungi Waliokamatwa Kati ya Mwaka 2011-2020……………………………………17

**Jedwali Na. 3**: Kiasi cha Heroin na Cocaine Kilichokamatwa Nchini Kati ya Mwaka 2011-2020……………………………………………..19

**Jedwali Na. 4**: Idadi ya Watuhumiwa wa Heroin na Cocaine Waliokamatwa Nchini Kati ya Mwaka 2011 – 2020………………………….20

**Jedwali Na. 5:** Aina na Idadi ya Sampuli za Dawa za Kulevya Zilizofanyiwa Uchunguzi……………………………………………………23

**Jedwali Na.6**: Kiasi na Aina ya Kemikali Bashirifu Zilizozuiwa Kuingia Nchini Kuanzia Mwaka (2017-2020)………………………24

**Jedwali Na. 7**: Kesi Zilizofikishwa Mahakamani Mwaka 2020 ........................ 26

**Jedwali Na. 8**: Asasi zilizotoa Elimu ya Dawa za Kulevya mwaka 2020 ...... 33

**Jedwali Na. 9**: Idadi ya Waraibu Waliopata Tiba kwenye Vitengo vya Afya ya Akili Nchini……………………………………………………35

**Jedwali Na.10**: Waraibu Waliohudumiwa na Kupewa Rufaa ya Methadone na Asasi za Kiraia, Januari hadi Desemba, 2020………...38

**Jedwali Na. 11:** Waraibu Waliopata Huduma katika Nyumba za Upataji Nafuu Mwaka 2020…………………………………………40

## ORODHA YA VIELELEZO

**Kielelezo Na. 1**: Kiasi cha Bangi na Mirungi Kilichokamatwa Nchini Kati ya Mwaka 2011-2020. ................................................................ 16

**Kielelezo Na. 2**: Mwenendo wa Kiasi cha Bangi na Mirungi Kilichokamatwa Nchini Kati ya Mwaka 2011-2020. ....................................... 17

**Kielelezo Na. 3**: Mwenendo wa Idadi ya Watuhumiwa Waliokamatwa kwa Kujihusisha na Bangi na Mirungi Nchini Kati ya Mwaka 2011 – 2020 ......................................................................... 18

**Kielelezo Na. 4:** Kiasi cha Heroin na Cocaine Kilichokamatwa Nchini Kati ya Mwaka 2011-2020. ................................................................ 19

**Kielelezo Na. 5**: Idadi ya Watuhumiwa wa Heroin na Cocaine Waliokamatwa Kati ya Mwaka 2011 - 2020. ................................................ 20

**Kielelezo Na. 6**: Mwenendo wa idadi ya Watuhumiwa Waliokamatwa Wakijihusisha na Heroin na Cocaine Kati ya Mwaka 2011 - 2020. ......................................................................................... 21

**Kielelezo Na. 7**: Dawa za kulevya kilo 268.50 zilizokamatwa Mbezi Kibanda cha Mkaa, Ubungo, Jijini Dar es Salaam, Aprili 2020 ....... 22

**Kielelezo Na. 8**: Uteketezaji wa dawa za kulevya aina ya heroin na bangi baada ya taratibu za Kisheria kukamilika ............................ 25

**Kielelezo Na. 9:** Kamishna Jenerali, James Kaji akitoa maelezo kwa Mgeni Rasmi, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa alipotembelea banda la Mamlaka siku ya kilele cha Maadhimisho ya Nanenane, mjini Bariadi Mkoani Simiyu, mwaka 2020.......................... 32

**Kielelezo Na. 10**: Kituo cha Tiba ya Methadone katika Hospitali ya Rufaa ya Mount Meru, jijini Arusha ...................................................... 39

**Kielelezo Na. 11**: Baadhi ya Waraibu wakipata Tiba ya methadone katika hospitali ya Mount Meru Arusha. ........................................ 39

# MAELEZO YA WAZIRI

Tatizo la Dawa za Kulevya lina madhara makubwa katika maisha ya wananchi, uwezo wa rasilimali watu na maendeleo endelevu ya Nchi yetu. Kwa kutambua athari hizo Serikali imeendelea kupambana na tatizo la dawa za kulevya kwa kuzuia biashara, kuimarisha utoaji wa elimu pamoja na upanuzi wa tiba kwa waathirika wa dawa hizo. Aidha, ushirikiano katika mapambano hayo umezidi kuimarishwa kitaifa, kikanda na kimataifa kwa kuwa tatizo hili ni mtambuka na linaathiri jamii yote na kuvuka mipaka ya Nchi yetu.

Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020-2025 inatambua umuhimu wa kupambana na tatizo la dawa za kulevya kwa kuwa tatizo hilo linaathiri watanzania katika nyanja zote muhimu ikiwemo afya, jamii, uchumi, mazingira, diplomasia pamoja na ulinzi na usalama wa Nchi yetu. Kwa muktadha huo,Ibara za 83 (t) na 244 (a) hadi 244 (l) zinasisitiza kuimarisha udhibiti na mapambano dhidi ya tatizo la dawa za kulevya kwa ajili ya ustawi wa Taifa letu.

Jitihada zilizofanyika kwa kipindi cha 2020 ni pamoja na kuvunja mitandao mikubwa ya wafanyabiashara ya dawa za kulevya na kufanya operesheni za ukamataji ambapo tani 13.2 za bangi, tani 11.8 za mirungi, kilo 349 za heroin na kilo 4.52 za cocaine zilikamatwa. Ukamataji huo ulihusisha jumla ya watuhumiwa 9,299 na kesi dhidi yao zilifikishwa Mahakamani, baadhi ya kesi zilisikilizwa na kutolewa maamuzi na nyingine zipo katika hatua mbalimbali za usikilizwaji. Vile vile, Serikali imeanza kuhamasisha kilimo cha mazao mbadala katika baadhi ya maeneo sugu ya kilimo cha bangi na mirungi.

Serikali imeendelea kuimarisha utoaji elimu, upanuzi wa huduma za tiba ya methadone na vitengo vya tiba vya afya ya akili na huduma za utengamao kwa ajili ya kuwasaidia waathirika wa dawa za kulevya. Sambamba na hayo, Serikali itaendelea kuboresha sheria, kanuni pamoja na miongozo mbalimbali ili kuongeza tija na ufanisi katika udhibiti wa dawa za kulevya.

Pamoja na udhibiti mkubwa wa dawa za kulevya unaofanywa na Serikali, kumejitokeza changamoto ya kubadilika mara kwa mara kwa njia na mifumo ya usafirishaji. Aidha, biashara ya dawa za kulevya imekuwa ikihusiana na makosa mengine ya kupanga na yanayovuka mipaka kama vile ugaidi, usafirishaji haramu wa binadamu, uuzaji haramu wa silaha, makosa ya kimtandao na utakatishaji fedha.

Serikali itaendelea kuimarisha ushirikiano na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya Nchi zikiwemo taasisi za kimataifa katika kupambana na tatizo la dawa za kulevya. Nawaomba wadau na wananchi wote kuendelea kutoa ushirikiano kwa Serikali katika mapambano dhidi ya tatizo la dawa za kulevya kwa manufaa ya ustawi wa Taifa letu.

Jenista Joakim Mhagama (Mb)
**Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu**
**(Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu)**

## DIBAJI

Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya ya Mwaka 2020 imeandaliwa kwa mujibu wa Kifungu cha 60 cha Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za kulevya Na 5 ya Mwaka 2015. Dhumuni la taarifa hii ni kuifahamisha jamii juu ya tatizo la dawa za kulevya lilivyokuwa Nchini kwa mwaka 2020 pamoja na jitihada zilizofanyika katika kukabiliana nalo.

Taarifa hii imegawanyika katika Sura Sita. Sura ya kwanza inaelezea tatizo la dawa za kulevya Duniani. Sura ya Pili inaelezea juu ya mikakati inayotumika katika kudhibiti na kupambana na tatizo la dawa za kulevya Nchini. Mikakati hiyo ni Kudhibiti Upatikanaji wa Dawa za Kulevya, Kupunguza Uhitaji wa Dawa za Kulevya, Kupunguza Madhara ya Matumizi ya Dawa za Kulevya na Kuimarisha Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa. Sura ya Tatu imejikita kwenye juhudi zilizofanyika katika kudhibiti uingizaji na usambazaji wa dawa za kulevya Nchini.

Sura ya Nne inafafanua mkakati wa Kupunguza Uhitaji wa Dawa za Kulevya Nchini. Jukumu la msingi katika mkakati huu ni kutoa Elimu kwa jamii ili ijiepushe na matumizi na biashara ya dawa za kulevya. Sura ya Tano imejikita katika kufafanua mkakati wa Kupunguza Madhara ya Matumizi ya Dawa za Kulevya. Sura ya Sita imeainisha changamoto na hatua za baadaye katika kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya Nchini.

Nawashukuru wadau wote walioshiriki kufanikisha maandalizi ya taarifa hii muhimu kwa jamii yetu. Tatizo la dawa za kulevya ni mtambuka hivyo linahitaji juhudi za pamoja katika kukabiliana nalo. Nachukua nafasi hii kuwaomba wadau wote kuimarisha ushirikiano katika udhibiti na mapambano dhidi ya tatizo la dawa la kulevya Nchini.

Gerald M. Kusaya
**KAMISHNA JENERALI**
**MAMLAKA YA KUDHIBITI NA**
**KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA**

# FAHARASA

| | |
|---|---|
| **ATS** | Aphetamine Type Stimulants |
| **COVID-19** | Coronavirus Disease |
| **GCLA** | Government Chemist Laboratory Agency |
| **INCB** | International Narcotics Control Board |
| **MAT** | Medication Assisted Treatment / Medical Assisted Treatment |
| **NPS** | New Psychoactive Substances |
| **PASADA** | Pastoral Activities and Services for People with AIDS Dar es Salaam Archdiocese |
| **TFS** | Tanzania Forest Services Agency |
| **TMDA** | Tanzania Medical and Drugs Authority |
| **UKIMWI** | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| **UNODC** | United Office on Drugs and Crime |
| **VVU** | Virusi Vya UKIMWI |
| **WHO** | World Health Organization |

# SURA YA KWANZA

# TATIZO LA DAWA ZA KULEVYA DUNIANI

## 1.1 Utangulizi

Sura hii inatoa taswira ya tatizo la dawa za kulevya Duniani ikiangazia matumizi, biashara, matibabu kwa waraibu na changamoto za udhibiti.Aidha sura hii inaonesha uhusiano uliokuwepo kati ya janga la virusi vya Corona (COVID-19) na tatizo la dawa za kulevya. Chanzo cha sura hii ni Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya ya Dunia ya Mwaka 2020.

## 1.2 Matumizi ya Dawa za Kulevya

Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya ya Dunia ya Mwaka 2020, inabainisha kuwa takribani watu wapatao milioni 269 wenye umri kati ya miaka 15 hadi 64 walitumia dawa za kulevya mwaka 2018. Bangi imeendelea kuwa dawa ya kulevya inayotumika zaidi Duniani ambapo mwaka 2018 ilitumiwa na watu milioni 192. Uhalalishaji wa uvutaji bangi katika nchi mbalimbali ulisababisha matumizi ya dawa hiyo kuongezeka. Hatahivyo, hadi kufikia mwaka 2019, asilimia 40 ya watumiaji wa bangi katika nchi zilizohalalisha bado walitumia bangi iliyotoka kwenye vyanzo visivyo halali.

Afyuni hususani heroin ilitumika na watu takribani milioni 30 wakati dawa za kulevya za jamii ya amphetamine na dawa tiba zenye asili ya vichangamshi zilitumika na watu wapatao milioni 27 katika mwaka 2018. Dawa tiba aina ya afyuni zenye asili ya kulevya hususani tramadol zimekuwa zikitumika zaidi katika nchi za Afrika ya Kaskazini, Kati na Magharibi. Hali hiyo inathibitishwa na ongezeko la waathirika wa dawa hiyo wanaotafuta tiba ya uraibu. Dawa za kulevya za jamii ya afyuni kama vile heroin zimekuwa zikisababisha madhara zaidi kwa watumiaji. Aidha, kati ya vifo 167,000 vilivyosababishwa na matumizi ya dawa za kulevya mwaka 2017, asilimia 66 vilisababishwa na matumizi ya afyuni. Katika kipindi cha muongo mmoja uliopita kumekuwa na dawa tofauti tofauti katika soko la dawa za kulevya Duniani. Katika muongo huo soko la dunia limeshuhudia kupanuka kwa wigo wa soko la dawa za kulevya mpya zikiwemo dawa tiba zenye asili ya kulevya.

## 1.3 Biashara ya Dawa za Kulevya Duniani

### Dawa za Viwandani

Dawa za viwandani zimechukua nafasi ya afyuni kwenye nchi ya Urusi na eneo la Asia ya katikatika kipindi cha muongo mmoja kutoka mwaka 2008 hadi 2018. Nchini Urusi kiasi cha afyuni kilichokamatwa kilipungua kwa asilimia 80 na waraibu waliokuwa wanatafuta tiba ya uraibu wa dawa hiyo nao walipungua ingawa kulikuwa na ongezeko la dawa za viwandani zenye asili ya vichangamshi aina ya methamphetamine na mephedrone. Hali hiyo ilienda sambamba na ongezeko la asilimia 70 la maabara haramu za kutengeneza dawa hizo kwenye miaka ya 2016 hadi 2018.

Tafiti zilizofanyika kwenye hospitali, magereza na taasisi mbalimbali nchini Iraq zilionesha methamphetamine ilikuwa ni dawa inayotumika zaidi kuliko bangi tangu mwaka 2012 ikifuatiwa na tramadol na captagon. Mamlaka za nchi ya Iraq pia ziliweza kubaini maabara haramu zilizojihusisha na utengenezaji wa methamphetamine. Aidha, Bodi ya Kimataifa ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya (INCB) nayo iligundua uingizaji nchini humo wa kiasi kikubwa wa kemikali bashirifu aina ya pseudoephedrine inayotumika kutengeneza methamphetamine.

Kemikali zilizozoeleka kuzalishia dawa za kulevya za aina ya amphetamine, methamphetamine na ecstasy zinadhibitiwa kimataifa. Wahalifu wanaozalisha dawa hizo wamebuni kemikali mbadala “designer precursors” kukwepa mkono wa sheria hivyo kuongeza changamoto katika udhibiti wa kemikali bashirifu.

### Dawa za Kulevya za Viwandani Jamii ya Amphetamine (ATS)

Dawa za kulevya za viwandani tofauti na ilivyo kwa dawa za kulevya zinazotokana na mimea kama heroin na cocaine, ni vigumu kukadiria kiasi kinachozalishwa. Ukamataji wa kiasi kikubwa cha tani 228 za methamphetamine mwaka 2018 ambao ulivunja rekodi unaashiria ongezeko la matumizi ya dawa hiyo. Nchi mbalimbali Duniani ziliharibu maabara bubu zipatazo 30,000 zilizokuwa zinazalisha dawa za jamii ya amphetamine ambapo asilimia 84 zilikuwa katika mabara ya Amerika.Aidha kiasi cha dawa

jamii ya amphetamine kilichokamatwa Duniani kimeongezeka katika kipindi cha miongo miwili hasa katika muongo wa pili (2009 – 2018).

**Dawa za Kulevya Jamii ya Afyuni (Opiates)**

Kilimo cha mimea ya afyuni Duniani kilipungua kwa asilimia 17 mwaka 2018 na kupungua zaidi kwa asilimia 30 mwaka 2019. Upungufu huo unachangiwa na kupungua kwa eneo lililotumika kulima mimea ya dawa hizo takribani hekta 240,800 katika nchi za Afghanistan na Myanmar. Hata hivyo, eneo linalotumika kulima mimea ya jamii ya afyuni Duniani ni kubwa ikilinganishwa na muongo mmoja uliopita.Ingawa eneo lililotumika kwa kilimo cha mimea ya afyuni Duniani lilipungua, kiasi cha afyuni kilichozalishwa mwaka 2019 hakikupungua. Aidha, bei ya dawa za kulevya jamii ya afyuni ikiwemo heroin katika nchi inayoongoza kwa uzalishaji ya Afghanistan ilipungua katika miaka ya 2018 na 2019. Kwa ujumla ukamataji wa dawa za kulevya jamii ya afyuni Duniani umebaki kuwa wa kiwango cha juu.

**Cocaine**

Kilimo cha mimea ya coca Duniani kilipungua kidogo kwa takribani hekta 244,200 ambazo ni sawa na punguzo la asilimia 0.5 mwaka 2018. Aidha, nchi ya Colombia imeendelea kuwa kinara katika kilimo cha mimea ya coca Duniani ambapo katika mwaka 2017 ilizalisha asilimia 70 ya majani ya mimea ya coca.Uzalishaji wa cocaine Duniani uliongezeka kwa asilimia 37 kati ya mwaka 2015 na 2016, asilimia 23 kati ya mwaka 2016 na 2017 na asilimia 4.6 kati ya mwaka 2017 na 2018.Ukamataji wa kiasi cha cocaine Duniani uliongezeka kwa asilimia 2.7 kufikia tani 1,311 mwaka 2018. Ongezeko la asilimia 71 la kiasi cha cocaine kilichokamatwa Duniani kwa kipindi cha muongo mmoja uliopita (2008 – 2018) linaashiria kuongezeka kwa uzalishaji wa dawa hiyo katika kipindi husika.

**Bangi**

Bangi tofauti na dawa zingine za mimea hulimwa karibu kila nchi Duniani kote ambapo takribani nchi 151 zilibainika kujihusisha na kilimo hicho kati ya mwaka 2010 na 2018. Kiasi cha bangi kinachokamatwa Duniani kinaonekana kupungua wakati idadi ya matukio ya ukamataji yakiongezeka. Matukio ya ukamataji bangi katika mwaka 2018 yalifikia milioni 1.4 Duniani

kote kwa mujibu wa Shirika linaloshughulikia masuala ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya na Uhalifu (UNODC).

Kiasi cha bangi kavu na bangi iliyosindikwa kilichokamatwa katika kipindi cha mwaka 2008 hadi 2018 kilipungua kwa asilimia 24 kufikia tani 5,610 mwaka 2018. Aidha kiwango kikubwa cha bangi kilikamatwa katika mabara ya Amerikaambapo Amerika kusini peke yake ilifanya asilimia 44 ya ukamataji wa Duniani kote. Ukamataji mkubwa Duniani wa bangi kavu kati ya mwaka 2008 na 2018 uliongozwa na nchi ya Marekani ikifuatiwa na Mexico, Paraguay, Colombia, Nigeria, Morocco, Brazil, India na Misri.

Kiasi kikubwa cha bangi iliyosindikwa kilichokamatwa katika kipindi cha mwaka 2008 hadi 2018 kilipatikana Hispania ikifuatiwa na Pakistani na Morocco. Morocco pekee imeripoti kuwa na takribani hekta 47,500 za bangi mwaka 2018. Afghanistan imeonekana kuwa nchi ya pili Duniani kwa kuzalisha bangi iliyosindikwa kwa kipindi cha mwaka 2014 hadi 2018 ikifuatiwa na Pakistani na Lebanon. Aidha kwa ujumla kiasi cha bangi iliyosindikwa kilichokamatwa kiliongezeka kwa mwaka 2018.

**Mwenendo wa Usafirishaji wa Dawa za Kulevya Duniani**

Wasafirishaji wa heroin, cocaine na methamphetamine wamebadili njia za usafirishaji wa dawa hizo. Kiasi cha heroin kilichokuwa kinasafirishwa kwa kutumia njia ya kaskazini kuelekea nchi ya Urusi kilipungua katika muongo mmoja kutoka asilimia 10 ya ukamataji heroin Duniani na kufikia asilimia moja mwaka 2018. Hata hivyo, ukamataji mkubwa uliofanyika karibuni kwenye njia hiyo unaonesha kuwa kwa sasa inatumika kusafirisha dawa hiyo kwenda Ulaya. Njia kuu ya usafirishaji heroin Duniani imeendelea kuwa ni ya Balkan, ikianzia nchi zalishaji ya Afghanistan, kupitia Iran na Uturuki na hatimaye kufikia masoko ya Ulaya ya Kati na Magharibi. Aidha, asilimia 58 ya heroin iliyokamatwa Duniani nje ya Afghanistan ilipitia njia hiyo mwaka 2018.

Vilevile, wafanyabiashara wa cocaine walibadili njia za usafirishaji ambapo nchi ya Venezuela ilikuwa ni kitovu cha usafirishaji wa dawa hiyo. Njia ya usafirishaji wa dawa hiyo ilibadilika baada ya kutokea machafuko ya kisiasa na kuanza kupitia nchi za Brazil na Uruguay. Mwaka 2019, Uruguay ilifanya

ukamataji wa tani tisa za cocaine, zilizokuwa zikisafirishwa kwenda Afrika ya Magharibi.

**Dawa Mpya za Kulevya**

Dawa mpya za kulevya ni dawa zinazotengenezwa kwa kuiga kemikali zilizoko kwenye dawa za kulevya zinazodhibitiwa kimataifa ili kuficha uhalisia wa dawa hizo kukwepa mkono wa sheria. Dawa hizi zina madhara sawa au zaidi ya dawa zinazodhibitiwa ya kimataifa. Pamoja na uwepo wa tatizo la matumizi ya dawa za kulevya zinazotokana na mimea tatizo liliongezeka kwa kuingizwa kwa dawa mpya za kulevya zisizodhibitiwa kimataifa.

Wastani wa dawa mpya za kulevya (New psychoactive substances) aina zipatazo 500 huingizwa sokoni kila mwaka. Dawa za kulevya za kundi la vichangamshi, ikifuatiwa na dawa za jamii ya bangi "cannabinoids" na kwa kiasi kidogo dawa za jamii ya afyuni zimetawala soko la dawa mpya za kulevya. Hatahivyo, kumekuwa na ongezeko la dawa mpya za kulevya za jamii ya afyuni hasa aina za fentanyl ambazo husababisha vifo vingi kwenye eneo la Amerika ya Kaskazini.

## 1.4 Matibabu kwa Waraibu wa Dawa za Kulevya

Inakadiriwa watu milioni 35.6 Duniani waliathirika kwa matumizi ya dawa za kulevya (drug use disorders) kwa mwaka 2018. Tafiti zinaonesha umasikini, elimu duni na unyanyapaa huongeza athari kwa watumiaji na kuwasababishia ukosefu wa ajira, kupoteza makazi na kunyanyapaliwa. Wanawake, wakimbizi na watu wanaoishi katika mazingira magumu huathirika zaidi na matumizi ya dawa za kulevya na huwawia vigumu kupata huduma za matibabu.

Watu milioni 11.3 walikadiriwa kujidunga dawa za kulevya mwaka 2018 ambao ni asilimia 10 ya watu waliokuwa na maambukizi ya VVU Duniani. Wajidunga zaidi ya milioni moja walikuwa wanaishi na maambukizi ya VVU, na wengine milioni 5.5 walikuwa na homa ya ini aina C. Kati ya vifo 585,000 vilivyotokana na matumizi ya dawa za kulevya mwaka 2017, nusu vilitokana na maambukizi ya homa ya ini aina C miongoni mwa wajidunga.

Huduma za matibabu kwa waraibu wa dawa za kulevya Duniani hazitoshelezi mahitaji ambapo kwa wastani mraibu mmoja kati ya wanane

hupata huduma hizo kwa mwaka. Theluthi moja ya waraibu ni wanawake, kwa wastani mwanamke mmoja hupata huduma ya matibabu ya uraibu kati ya watu watano. Idadi ya wanawake wanaopata huduma za matibabu ni wachache zaidi ikilinganishwa na wanaume.

Madhara yaliyosababishwa na matumizi ya dawa za kulevya kwa ujumla yaliongezeka Duniani katika kipindi cha muongo mmoja kuanzia mwaka 2007 hadi 2018 kwa kuongeza vifo vinavyozuilika na kushusha uzalishaji. Mfano, kipindi hicho, saratani ya ini iliongeza vifo kwa asilimia 40 miongoni mwa wajidunga wa dawa za kulevya kutokana na wengi wao kuwa na maambukizi ya virusi vya homa ya ini aina C.

## 1.5 Changamoto za Udhibiti wa Tatizo la Dawa za Kulevya

**Matibabu**

Mahitaji ya huduma za matibabu kwa waraibu wa dawa za kulevya Duniani ni makubwa ikilinganishwa na huduma zinazotolewa ambapo kwa wastani mraibu mmoja kati ya wanane hupata huduma hizo kwa mwaka. Aidha, theluthi moja ya waraibu ni wanawake, kwa wastani mwanamke mmoja hupata huduma ya matibabu ya uraibu kati ya watu watano. Vilevile, janga la virusi vya Corona (COVID-19) liliongeza changamoto ya waraibu wa dawa za kulevya kuweza kupata huduma za matibabu na kujikuta wakiathirika zaidi na dawa hizo.

**Upungufu wa Rasilimali Fedha**

Serikali Duniani zimekuwa zikitenga bajeti ndogo ikilinganishwa na mahitaji halisi ya udhibiti wa dawa za kulevya ambapo mwaka 2000 bajeti ilipungua kutoka asilimia tatu hadi 0.02 mwaka 2017. Halikadhalika, bajeti halisi zinazotumika kwenye udhibiti wa dawa za kulevya zimepungua kutoka asilimia 1.9 mwaka 2003 hadi 0.04 mwaka 2017.

**Kudhoofika kwa Operesheni za Pamoja za Kimataifa**

Operesheni za pamoja za kimataifa za udhibiti wa dawa za kulevya Duniani zilipungua kutoka ushiriki wa nchi 68 mwaka 2010 hadi kufikia nchi 58 mwaka 2018. Mdororo wa uchumi wa mwaka 2008 unatajwa kama sababu

kuu ambapo fedha za udhibiti zilipunguzwa kwa kiasi kikubwa. Vilevile kukosekana kwa mikataba ya kuongoza operesheni, kushindwa kutambua wadau muafaka na tofauti za lugha ziliathiri operesheni hizo.

## 1.6 Janga la Virusi vya Corona (COVID-19)

Biashara haramu ya dawa za kulevya hufanyika kwa kificho kwa kutumia mfumo halali wa biashara. Hatua zilizochukuliwa katika kudhibiti janga la virusi vya Corona ziliathiri biashara pamoja na mzunguko mzima wa dawa za kulevya. Nchi mbalimbali Duniani zimeripoti uhaba wa dawa za kulevya zinazouzwa mitaani, kuongezeka kwa bei ya dawa za kulevya, kupungua kwa ubora wa dawa zinazouzwa na watumiaji kuanza kutumia dawa mbadala za kulevya.

Nchi za Balkan na Mashariki ya Kati ambazo hazikuchukua hatua kali katika kudhibiti janga la virusi vya Corona hazikupata mabadiliko katika biashara ya dawa za kulevya. Udhibiti wa janga la virusi vya Corona umechangia katika kupunguza kiasi cha dawa za kulevya zilizokamatwa katika nchi za Italia, Niger na zile za Asia ya Kati ingawa kwa upande mwingine uliongeza uhalifu wa kimtandao kwa kuuza dawa bandia kwenye nchi za Balkan.

### 1.6.1 Uzalishaji wa Dawa za Kulevya

**Kilimo na Biashara ya Afyuni**

Uvunaji afyuni mwaka 2020 nchini Afghanistan ulikumbana na kadhia ya janga la virusi vya Corona na kusababisha kupungua kwa nguvu kazi kutoka nchi jirani ya Pakistani. Hata hivyo wanawake na watu wengine waliopoteza ajira nchini Afghanistan kutokana na janga hilo walitumia fursa hiyo ya uvunaji afyuni hali iliyosababisha uvunaji kutoathirika.

Kemikali bashirifu aina ya acetic anhydride ambayo ni muhimu kwa uzalishaji wa heroin iliripotiwa kuadimika nchini Afghanistan kutokana na vikwazo vya janga la virusi vya Corona. Hali hiyo iliweza kusababisha kushuka kwa uzalishaji wa heroin kwenye nchi hiyo inayoongoza katika uzalishaji wa dawa hiyo Duniani.

Nchi ya Myanmar inayofuatia kwa uzalishaji wa heroin Duniani, ilifanikiwa kuvuna afyuni kabla ya janga la virusi vya Corona ingawa ilikumbana na changamoto ya kukosa soko kutokana na vikwazo vya biashara vilivyotokana na janga hilo. Hata hivyo, hakuna ushahidi wa kuathirika kwa uzalishaji wa afyuni katika nchi ya Mexico.

**Uzalishaji wa Cocaine**

Hatua zilizochukuliwa katika kudhibiti janga la virusi vya Corona, hazikuathiri jitihada za kudhibiti uzalishaji wa cocaine Duniani hasa katika nchi ya Colombia ambayo ni mzalishaji mkuu wa dawa hiyo Duniani.

Kwa upande wa nchi ya Bolivia ambayo ni moja ya wazalishaji wakubwa wa cocaine Duniani, machafuko ya kisiasa yaliyotokea mwishoni mwa mwaka 2019 pamoja na janga la virusi vya Corona, vimeifanya serikali ya nchi hiyo kushindwa kudhibiti kilimo cha mimea ya coca nchini humo.

Nchi ya Peru ambayo ni mzalishaji mwingine mkubwa wa cocaine Duniani imejikuta ikikosa soko la cocaine na hatimaye ikashuka bei. Hali hiyo inaweza kusababisha kushuka kwa uzalishaji wa cocaine walau kwa kipindi kifupi nchini humo. Kwa ujumla, mdororo wa uchumi unaotokana na vikwazo vya COVID-19 unatarajiwa kuongeza uzalishaji wa cocaine katika maeneo haya katika siku za usoni.

**Upatikanaji wa Kemikali Bashirifu**

Janga la virusi vya Corona halikuathiri uzalishaji wa dawa za kulevya za kutengenezwa kwenye nchi za Kusini Mashariki mwa Asia na Urusi ambazo huzalisha kemikali bashirifu. Hata hivyo, janga la virusi vya Corona vilifanya kemikali bashirifu kutoka nchi za Kusini Mashariki mwa Asia kuathiri uzalishaji wa methamphetamine na fentanyl nchini Mexico, uzalishaji wa ATS aina ya captagon kwenye nchi za Lebanon na Syria pamoja uzalishaji wa methamphetamine nchini Czechia (Jamhuri ya Ucheki).

Aidha, janga hilo liliwaathiri watumiaji wa kemikali bashirifu na kusababisha bei ya dawa za kulevya kupanda. Mfano, uhaba wa kemikali bashirifu za kuzalishia dawa ya kulevya aina ya methamphetamine kutoka eneo la Asia Mashariki ulisababisha ongezeko la bei ya dawa hiyo kwenye nchi za Mexico na Marekani kwa mwezi Machi, 2020.

### 1.6.2 Usafirishaji wa Dawa za Kulevya

**Usafirishaji kwa Njia ya Anga**

Usafirishaji wa dawa za kulevya kwa njia ya anga umeathirika kwa kiwango kikubwa kutokana na janga la virusi vya Corona. Usitishaji wa usafiri wa anga kama moja ya hatua ya kudhibiti kuenea kwa virusi hivyo, kuliathiri usafirishaji wa dawa za kulevya zilizokuwa zinategemea njia hiyo hasa kwa dawa za kutengenezwa hususani metamphetamine.

Nchi zinazotegemea dawa za kulevya zinazoingizwa kwa njia ya anga kama Japan, Korea na Australia zilitarajiwa kuathirika zaidi. Aidha, dawa nyingine za kulevya ikiwemo heroin ilikuwa ikisafirishwa zaidi kwa njia ya barabara ikichanganywa na bidhaa nyingine halali, wakati cocaine imekuwa ikisafirishwa zaidi kwa njia ya maji kwa kutumia vyombo binafsi.

**Usafirishaji kwa Njia ya Maji**

Kulikuwa na ongezeko la usafirishaji wa heroin kwa njia ya maji baada ya hatua za kudhibiti virusi vya Corona kuathiri njia ya barabara iliyokuwa inatumika awali. Hali hii ilidhihirika kwenye nchi ya Iran na eneo la Asia ya Kati. Ukamataji wa heroin niliyokuwa inasafirishwa kutoka Afghanistan kwenda Ulaya kwa kupitia njia ya Kusini uliongezeka katika Bahari ya Hindi.

Kadhalika hatua za kudhibiti janga la Corona zimekwamisha usafirishaji cocaine kwenda nchi za Ulaya kwa njia anga. Hivyo, kumekuwa na ongezeko la usafirishaji cocaine kutoka nchi za Amerika ya Kusini kwenda nchi za Ulaya kwa kutumia vyombo vya majini. Nchi ya Colombia ambayo ni mzalishaji mkubwa wa cocaine imeripoti ongezeko la usafirishaji wa dawa hiyo kwa njia ya maji badala njia ya barabara iliyokuwa inatumika zaidi awali. Vilevile, ongezeko la kiasi cha cocaine kilichokamatwa hivi karibuni katika bandari za nchi za Ulaya inadhihirisha kuwepo kwa usafirishaji wa kiasi kikubwa cha cocaine kwa njia ya maji.

**Usafirishaji kwa Njia ya Barabara**

Udhibiti mkali wa usafirishaji wa watu na bidhaa kwa njia ya barabara hasa katika maeneo ya mipakani kama hatua za kudhibiti janga la Corona umesaidia kuzuia usafirishaji wa heroin kwenda Marekani. Hali hiyo,

imesababisha bei ya afyuni inayozalishwa nchini Myanmar kushuka kutokana na kushindikana kuvushwa mipakani kwenda nchi za Mashariki mwa Asia.

**Mrundikano wa Dawa za Kulevya**

Mkanganyiko uliojitokeza kwenye biashara ya dawa za kulevya kutokana na vikwazo vya janga la virusi vya Corona unaweza kusababisha mrundikano wa dawa za kulevya zinazosubiri kuingizwa sokoni. Kuporomoka kwa bei ya dawa hizo ni ushahidi wa kuwepo kwa hali hiyo. Mrundikano wa dawa za kulevya unaweza kusababisha ongezeko la ghafla la kiasi cha dawa za kulevya zinazoingia sokoni mara vikwazo vya janga la virusi vya Corona vitakapoondolewa. Hali hiyo pia inaweza kushusha bei ya dawa za kulevya ambazo hazijachakachuliwa 'pure' na kuleta athari inayotokana na kuzidisha kiasi cha dawa za kulevya kinachotumika kwa mara moja 'overdose'.

**Biashara na Matumizi ya Bangi**

Kiasi kikubwa cha bangi na bidhaa zake kilichokamatwa kwenye nchi za Afrika Kaskazini na Mashariki kinaonesha janga la virusi vya Corona halikuathiri usafirishaji bangi iliyosindikwa kwenda Ulaya. Kuna viashiria kuwa masharti ya kujifungia ndani kudhibiti maambukizi ya virusi vya Corona yamechangia katika kuongeza mahitaji ya bangi na hivyo kutoa fursa ya ongezeko la biashara ya bangi kutoka Afrika kwenda Ulaya. Biashara ya bangi haikutetereka kwa kuwa inalimwa karibu na maeneo inapotumika na hivyo haihitaji usafirishaji wa masafa marefu kama ilivyo kwa heroin na cocaine.

**Biashara ya Dawa za Kulevya Kupitia Mtandao wa Siri 'Darknet'**

Hatua za kudhibiti janga la Corona zimewafanya watumiaji wa dawa za kulevya kushindwa kukutana na wauzaji wa dawa hizo kwa urahisi. Hivyo baadhi ya watumiaji wa dawa za kulevya waliamua kununua dawa hizo kwa njia ya mtandao wa siri pamoja na njia ya vifurushi. Ingawa usafirishaji wa bidhaa kwa njia ya posta kimataifa umeathiriwa na janga la virusi vya Corona, hata hivyo kuna viashiria kuwa katika robo ya kwanza ya mwaka 2020 biashara ya dawa za kulevya iliongezeka katika mitandao mitatu ya siri iliyopo Ulaya.

**Wafanyabiashara wa Dawa za Kulevya**

Kuna uwezekano mkubwa wa serikali mbalimbali Duniani kutumia rasilimali zilizokuwa zielekezwe katika kudhibiti tatizo la dawa za kulevya kupambana na janga la virusi vya Corona. Hali hiyo inatoa mwanya wa kushamiri kwa kilimo, uzalishaji na biashara ya dawa za kulevya. Aidha, baadhi ya wafanyabiashara wa dawa za kulevya wametumia fursa ya kudhibititi janga la virusi vya Corona kujisafisha kwa kuunga mkono jitihada za kudhibiti janga hilo hususani kwenye jamii masikini.

### 1.6.3 Matumizi ya Dawa za Kulevya

Matumizi ya dawa za kulevya Duniani ni makubwa zaidi katika jamii zenye uwezo mkubwa kiuchumi ingawa madhara huwa makubwa zaidi kwa jamii maskini. Janga la virusi vya Corona lililopunguza ajira na kuleta umaskini, linawaweka watu wengi zaidi katika hatari ya kudhurika na matumizi ya dawa za kulevya. Aidha, uhaba wa dawa za kulevya unaotokana na janga la virusi vya Corona unaongeza hatari za kiafya kwa waraibu.

**Matumizi ya Dawa Mbadala**

Nchi za Ulaya, Kusini Mashariki mwa Asia na Amerika ya Kaskazini zimemeripoti upungufu wa heroin iliyokuwa inauzwa rejareja. Hali hiyo inaenda sambamba na kupungua kwa matumizi ya dawa za kulevya. Watumiaji hujikuta wakilazimika kutumia dawa za kulevya mbadala zinazopatikana kwenye mazingira yao na kujiweka katika hatari zaidi kiafya. Nchi za Ulaya zilitoa taarifa ya uwezekano wa watumiaji wa heroin kuanza kutumia dawa za jamii ya fentanyl. Matumizi ya dawa tiba zenye asili ya kulevya hasa za kundi la benzodiazepine na buprenorphine yameongezeka na kusababisha bei ya dawa hizo kupanda maradufu.Vilevile dawa za kutengeneza na pombe zimeonekana kutumika kama mbadala wa dawa za jamii ya afyuni.

**Ongezeko la Wajidunga**

Baadhi ya watumiaji wa dawa za kulevya walianza kujidunga dawa hizo na kujiongezea uwezekano wa kuambukizana VVU, virusi vya homa ya ini aina C na COVID-19 pale wanaposhirikiana vifaa wanavyojidungia. Janga la virusi vya Corona liliathiri taasisi zilizokuwa zinatoa tiba kwa waraibu kwa kushindwa kutoa huduma hizo kwa ufanisi. Hali hiyo ilisababisha baadhi ya

nchi kulegeza masharti ya utolewaji wa huduma hizi ikiwemo Uingereza iliyoruhusu maduka ya dawa kutoa dawa ya methadone na nchi zingine kuruhusu matumizi ya methadone nyumbani 'take-away doses'.Ongezeko la wajidunga linaweza kufananishwa na madhara ya mdororo wa uchumi wa mwaka 2008 ambapo serikali zilipunguza rasilimali za udhibiti wa tatizo la dawa za kulevya na kusababisha ongezeko la matumizi ya dawa hizo.

**Vifo kwa Waraibu**

Maambukizi ya virusi vya Corona yanaongeza matatizo ya kiafya kwa waraibu ambao kwa kawaida huwa na changamoto nyingi za kiafya. Watumiaji wa vipumbaza husumbuliwa zaidi na matatizo ya kiafya ya njia ya hewa na wale wanaotumia vichangamshi hushambuliwa zaidi na magonjwa ya mapafu. Watumiaji huwa na kinga ndogo ya mwili ya kupambana na maradhi na kuwa katika hatari ya kupata maradhi ya moyo. Changamoto hizo za kiafya huwaweka waraibu wa dawa za kulevya katika hatari ya kupoteza maisha pale wanapopata maambukizi ya virusi vya Corona.

# SURA YA PILI

# MIKAKATI YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA NCHINI

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea juu ya mikakati inayotumika katika kudhibiti na kupambana na tatizo la dawa za kulevya Nchini. Mikakati hiyo ni kudhibiti upatikanaji wa dawa za kulevya, kupunguza uhitaji wa dawa za kulevya, kupunguza madhara ya matumizi ya dawa za kulevya na kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa.

## 2.2 Kudhibiti Upatikanaji wa Dawa za Kulevya (Supply Reduction)

Mkakati wa kwanza katika kudhibiti na kupambana na dawa wa kulevya ni kudhibiti uzalishaji na usambazaji wa dawa za kulevya Nchini. Katika utekelezaji wa mkakati huo, Mamlaka imejikita katika Ukusanyaji na uchambuziwa taarifa za wanaojihusisha na dawa za kulevya; Ukamataji wa wafanyabiashara wa dawa za kulevya;Kudhibiti uzalishaji wa dawa za kulevya (Kilimo na Uzalishaji);Kudhibiti uchepushwaji wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevyapamoja na Kuandaa na kusimamia miongozo ya uteketezaji wa dawa za kulevya.

## 2.3 Kupunguza Uhitaji wa Dawa za Kulevya (Demand Reduction)

Mkakati huu ni wa pili unaolenga katika utoaji wa elimu kwa jamii ili kuiepusha isiingie katika matumizi na biashara ya dawa za kulevya.Mkakatihuu unatekelezwa kwa kutoa elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya katika jamii,kuandaa miongozo ya uelimishaji na kuwaandaa walimu wa walimu.

## 2.4 Kupunguza Madhara ya Matumizi ya Dawa za Kulevya (Harm Reduction)

Mkakati wa tatu umejikita katika utoaji wa tiba na ushauri kwa waraibu wa dawa za kulevya pamoja na jamii inayowazunguka. Lengo ni kuhakikisha waraibu wa dawa hizo wanapata tiba hivyo kupunguza madhara ya kiafya, kijamii na kiuchumi. Katika kutekeleza mkakati huumiongozo ya matibabu huandaliwa, uratibu wa matibabu kwa waathirika wa dawa za kulevya

pamoja na kufanya usimamizi shirikishi katika vituo vinavyotoa huduma za tiba kwa waathirika wa dawa za kulevya.

### 2.5 Kuimarisha Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

Mkakati huu wa nne unalenga katika kuimarisha ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa kwa kuwa tatizo la dawa za kulevya hasa biashara ya dawa za kulevya ni suala mtambuka na biashara inayofanyika bila mipaka. Maeneo ya msingi ya mkakati huu ni Kutekeleza mikataba na miongozo ya kimataifa katika udhibiti wa dawa za kulevya; Kushiriki mikutano ya kimataifa kuhusu udhibiti wa dawa za kulevya; Kubadilishana taarifa na mataifa mbalimbali kuhusu udhibiti wa dawa za kulevya na kushirikisha wadau mbalimbali ndani na nje ya nchi katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

# SURA YA TATU

# KUDHIBITI UPATIKANAJI WA DAWA ZA KULEVYA

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea juhudi zilizofanyika katika kudhibiti upatikanaji wa dawa za kulevya nchini kwa kipindi cha kuanzia Januari hadi Desemba, 2020.

## 3.2 Udhibiti wa Upatikanaji wa Dawa za Kulevya

Tanzania iliendelea na juhudi za kudhibiti na kupambana na tatizo la dawa za kulevya za mashambani kama vile bangi na mirungi pamoja na zilizozalishwa viwandani zikiwemococaine na heroin.Katika kipindi hicho jumla ya kesi **7,361** za dawa za kulevya ziliripotiwa nchini. Kati ya hizo, kesi **428** zilihusu dawa za kulevya za viwandani na kesi **6,933** zilihusu dawa za kulevya za mashambani. Aidha, watuhumiwa **508** walikamatwa na dawa za kulevya za viwandani na watuhumiwa **8,757** walikamatwa na dawa za kulevya za mashambani. Mchanganuo wa dawa hizo ni kama ifuatavyo:

### Bangi

Kiasi cha tani **13.23** za bangi zilikamatwa na kuhusisha jumla ya watuhumiwa **7,601.** Aidha, jumla ya mashamba ya bangi **28** yenye ukubwa wa ekari **26.2** yakihusisha watuhumiwa **34** yalikamatwa na kuteketezwa kwa mujibu wa sheria. (***Jedwali Na.1 na Kielelezo Na.1).***


### Mirungi

Tani **11.80** za mirungi zilikamatwa zikihusisha watuhumiwa **1,156**. Aidha, mifumo ya kieletroniki ambayo ni *Precursors Incident Communication System* (PICS), na *Project Ion* (IONICS) ilisaidia kwa kiasi kikubwa kubaini na kukamata mirungi iliyokuwa inasafirishwa kwa njia ya vifurushi kutoka nchi ya Ethiopia kupitia Tanzania kwenda Amerika ya Kaskazini. **(*Rejea Jedwali Na.1 na Kielelezo Na.1).***


**Jedwali Na. 1: Kiasi cha Bangi na Mirungi Kilichokamatwa Nchini Kati ya Mwaka 2011-2020.**

| Mwaka | Bangi (Tani) | Mirungi (Tani) |
|---|---|---|
| 2011 | 17.30 | 0.10 |
| 2012 | 48.70 | 6.22 |
| 2013 | 85.80 | 12.82 |
| 2014 | 81.30 | 15.74 |
| 2015 | 22.01 | 16.60 |
| 2016 | 68.23 | 21.64 |
| 2017 | 52.19 | 67.81 |
| 2018 | 24.30 | 8.96 |
| 2019 | 21.51 | 9.07 |
| 2020 | 13.23 | 11.80 |

**Kielelezo Na. 1: Kiasi cha Bangi na Mirungi Kilichokamatwa Nchini Kati ya Mwaka 2011-2020.**



**Kielelezo Na. 2: Mwenendo wa Kiasi cha Bangi na Mirungi Kilichokamatwa Nchini Kati ya Mwaka 2011-2020.**





Takwimu zinaonesha kiasi cha bangi kilichokamatwa kiliendelea kupungua kuanzia mwaka 2017 mpaka 2020, hii ni kutokana na kuimarika kwa jitihada za udhibiti. Halikadhalika, kiasi cha mirungi kilichokamatwa mwaka 2020 kiliongezeka ikilinganishwa na mwaka 2019 kutokana na kubainika kwa mtandao wa usafirishaji wa dawa hizo kutokea nchini Ethiopia kupitia Tanzania kwenda Ulaya, Marekani na Canada kwa njia ya Posta.

**Jedwali Na. 2: Idadi ya Watuhumiwa wa Bangi na Mirungi Waliokamatwa Kati ya Mwaka 2011-2020**

| Mwaka | Idadi ya Watuhumiwa – Bangi | Idadi ya Watuhumiwa – Mirungi |
|---|---|---|
| 2011 | 39 | 100 |
| 2012 | 5,548 | 847 |
| 2013 | 1,547 | 581 |
| 2014 | 11,918 | 1,650 |
| 2015 | 13,275 | 1,780 |
| 2016 | 17,889 | 2,397 |
| 2017 | 11,528 | 1,797 |

| | | |
|---|---|---|
| 2018 | 9,744 | 1,185 |
| 2019 | 8,865 | 1,170 |
| 2020 | 7,601 | 1,156 |

**Kielelezo Na. 3: Mwenendo wa Idadi ya Watuhumiwa Waliokamatwa kwa Kujihusisha na Bangi na Mirungi Nchini Kati ya Mwaka 2011 – 2020**




Kielelezo Namba 3 kinaonesha idadi ya watuhumiwa wa bangi na mirungi kwa mwaka 2020 imeendelea kupungua ikilinganishwa na miaka iliyopita hii ni kutokana na juhudi kubwa zinazofanyika katika udhibiti.

**Heroin**

Jumla ya kilo **349.81** za heroin zilikamatwa Nchini zikiwahusisha watuhumiwa **428.** (***Rejea Jedwali Na.3 na Kielelezo Na.4)***.


**Cocaine**

Kiasi cha kilo **4.52** za cocaine zilikamatwa zikiwahusisha watuhumiwa **80.**(***Rejea Jedwali Na.3 na Kielelezo Na.4)***.

**Jedwali Na. 3: Kiasi cha Heroin na Cocaine Kilichokamatwa Nchini Kati ya Mwaka 2011-2020.**

| Mwaka | Kiasi cha Heroin kilichokamatwa (Kg) | Kiasi cha Cocaine kilichokamatwa (Kg) |
|---|---|---|
| 2011 | 264.26 | 128 |
| 2012 | 260 | 151 |
| 2013 | 36 | 4 |
| 2014 | 400 | 45 |
| 2015 | 64.75 | 17.79 |
| 2016 | 42.26 | 18.52 |
| 2017 | 185.56 | 4.14 |
| 2018 | 16.94 | 7.67 |
| 2019 | 55.35 | 10.34 |
| 2020 | 349.81 | 4.52 |

**Kielelezo Na. 4: Kiasi cha Heroin na Cocaine Kilichokamatwa Nchini Kati ya Mwaka 2011-2020.**





Takwimu zinaonesha kiasi cha heroin kilichokamatwa kwa mwaka 2020 kimeongezeka mara sita zaidi ikilinganishwa na mwaka 2019. Hali hii

ilitokana na kutumika kwa mbinu mpya na ushirikiano wa kimataifa katika kuwabaini na kuwakamata wafanyabiashara wakubwa ambao mara nyingi hukutwa na kiasi kikubwa cha dawa hizo.

**Jedwali Na. 4: Idadi ya Watuhumiwa wa Heroin na Cocaine Waliokamatwa Nchini Kati ya Mwaka 2011 - 2020**


| Mwaka | Watuhumiwa - Heroin | Watuhumiwa - Cocaine |
|---|---|---|
| 2011 | 20 | 30 |
| 2012 | 400 | 138 |
| 2013 | 75 | 20 |
| 2014 | 584 | 351 |
| 2015 | 474 | 281 |
| 2016 | 716 | 263 |
| 2017 | 1,005 | 243 |
| 2018 | 463 | 148 |
| 2019 | 318 | 31 |
| 2020 | 428 | 80 |

**Kielelezo Na. 5: Idadi ya Watuhumiwa wa Heroin na Cocaine Waliokamatwa Kati ya Mwaka 2011 - 2020.**



Kielelezo Na. 5 kinaonesha idadi ya watuhumiwa waliokamatwa na Heroin na Cocaine kwa mwaka 2020 iliongezeka ikilinganishwa na mwaka 2019. Hali hii inatokana na kuongezeka kwa ushirikiano kati ya vyombo vya dola na jamii uliosaidia kupatikana kwa taarifa zilizowezesha kubaini mitandao ya wafanyabiashara wakubwa wa dawa hizo.

**Kielelezo Na. 6: Mwenendo wa Idadi ya Watuhumiwa Waliokamatwa Wakijihusisha na Heroin na Cocaine Kati ya Mwaka 2011 - 2020.**






***Kielelezo Na. 7****: Dawa za kulevya kilo 268.50 zilizokamatwa Mbezi Kibanda cha Mkaa, Ubungo, Jijini Dar es Salaam, Aprili 2020*

### 3.3 Uchunguzi wa Kimaabara wa Dawa za Kulevya

Uchunguzi wa kimaabara wa dawa za kulevya ni mojawapo ya matakwa ya kisheria katika kuthibitisha aina za dawa zinazokamatwa. Katika kufanikisha hilo sampuli zilizokamatwa zinazodhaniwa kuwa za dawa za kulevya hupelekwa kwenye maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Katika kipindi cha Mwaka 2020, jumla ya sampuli 43,018 zilifanyiwa uchunguzi, kati ya hizo, sampuli 42,705 zilibainika kuwa dawa za kulevya ambazo ni sawa na asilimia 99.3. Aidha, dawa za kulevya aina ya bangi zilikuwa asilimia 91, heroin asilimia 6, na mirungi asilimia 3. Aina ya sampuli na idadi ya aina mbalimbali za dawa za kulevya zimeainishwa katika Jedwali Na 5.

**Jedwali Na. 5: Aina na Idadi ya Sampuli za Dawa za Kulevya Zilizofanyiwa Uchunguzi**

| Aina ya Sampuli | Idadi ya Sampuli |
|---|---|
| Bangi | 38,721 |
| Heroin | 2,402 |
| Mirungi | 1,417 |
| Cocaine | 3 |
| Lorazepam | 4 |

### 3.4 Udhibiti wa Kemikali Bashirifu

Kemikali bashirifu ni kemikali ambazo pamoja na matumizi mengine halali zinaweza kuchepushwa na kutumika kutengeneza dawa za kulevya. Matumizi halali ya kemikali hizo ni pamoja na kutengenezea bidhaa mbalimbali viwandani na shughuli za kimaabara. Katika kipindi Januari hadi Desemba, 2020 kiasi cha lita za ujazo **3,142,945.67** na **kilo 2,722.12** za kemikali bashirifu ziliingizwa nchini kwa mujibu wa Sheria. Kemikali hizo zilifanyiwa ufuatiliaji ili zisichepushwe kutengeneza dawa za kulevya.

Udhibiti wa uchepushwaji wa kemikali bashirifu, ulifanyika kwa kufanya ukaguzi katika maeneo **45** katika mikoa ya Dar es salaam, Pwani, Morogoro, Geita, Shinyanga, Mwanza na Kilimanjarona mipaka yaNamanga, Tarakea, Holili, Manyovu, Mabamba, Kasumulu na Tunduma. Ukaguzi huo ulihusisha kampuni zinazoingiza, kusambaza nakutumia kemikali bashirifu pamoja na zinazosafirisha vifurushi likiwemo Shirika la Posta Nchini.

Matokeo ya ukaguzi yalibainisha kuwa, baadhi ya kampuni hazikuwa na kumbukumbu zinazojitosheleza kuhusu mwenendo wa usambazaji na matumizi ya kemikali na hivyo kutoa mwanya wa uwezekano wa uchepushwaji. Vilevile, baadhi ya wafanyabiashara walibainika kutokuwa na ufahamu juu madhara ya uchepushwaji wa kemikali bashirifu.

Udhibiti wa kemikali bashirifu mwaka 2020 ulifanikisha kuzuia uingizaji wa tani 57.6 za kemikali bashirifu aina ya toluene ambazo zilikuwa ziingizwe Nchini kinyume cha sharia. Udhibiti huo ulifanikishwa kwa kutumia mifumo ya kieletroniki ya Pre –Export Notification System (PEN) inayoratibiwa na Bodi ya Kimataifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevya (INCB).

***Jedwali Na. 6:*** **Kiasi na Aina ya Kemikali Bashirifu Zilizozuiwa Kuingia Nchini Kuanzia Mwaka (2017-2020)**

| Mwaka | Kemikali Bashirifu zilizozuiwa kuingizwa Nchini | Kiasi (Kg) |
|---|---|---|
| 2017 | Acetone | 3.90 |
| | Methyl ethyl ketone (MEK) | 250,076.50 |
| | Hydrochloric acid | 37 |
| 2018 | Acetone | 6,480 |
| | Methyl ethyl ketone (MEK) | 46 |
| | Hydrochloric acid | 10,100 |
| | Sulphuric acid | 10,100 |
| | Toluene | 6,480 |
| 2019 | Acetone | 7.90 |
| | Toluene | 23,628 |
| | Hydrochloric acid | 20,000 |
| | Ethyl ether | 3.54 |
| 2020 | Toluene | 57,600 |

## 3.5 Udhibiti wa Dawa Tiba Zenye Asili ya Kulevya

Kuimarika kwa udhibiti wa dawa za kulevya kama vile heroin na cocaine kumesababisha watu kujihusisha na matumizi ya dawa tiba zenye asili ya kulevya kama mbadala wa dawa hizo hasa katika maeneo ya mijini. Udhibiti wa dawa tiba zenye asili ya kulevya ulifanyika mwaka 2020 ambapo kampuni na maduka 77 yalikaguliwa katika ya mikoa ya Tanga, Dar es Salaam, Shinyanga (Kahama), Geita, Arusha, Morogoro, Kilimanjaro, Manyara na Dodoma (Kondoa). Aidha, ukaguzi huo ulibaini uwepo wa uhitaji mkubwa wa dawa hizo kwa matumizi haramu, kutokuwepo kwa kumbukumbu za matumizi ya dawa hizo, kutolewa bila cheti cha daktari pamoja na utunzaji holela wa dawa tajwa. Katika kipindi cha mwaka 2020 zaidi ya kilo 762 za dawa tiba zenye asili ya kulevya ziliingizwa nchini kihalali ambazo zilifuatiwa kwa karibu ili zisichepushwe.

### 3.6 Ushirikiano Katika Udhibiti wa Kemikali Bashirifu na Dawa Tiba Zenye Asili ya Kulevya

Wadau mbalimbali wameendelea kushirikiana mwaka 2020 wakiongozwa na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya. Wadau hao ni pamoja na Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Mamlaka ya Dawa na Vifaa tiba, Bohari Kuu ya Dawa, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Ushirikiano huo ambao ulihusisha kubadilishana taarifa na kufanya operesheni za pamoja za kudhibiti uchepushwaji wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya ulifanikisha kukamata na kuteketeza kemikali bashirifu kilo 50 aina ya ephedrine hydrochloride.

### 3.7 Uteketezaji wa Dawa za Kulevya

Dawa za Kulevya zinazokamatwa huteketezwa kwa mujibu wa sheria kwa kushirikisha Mamlaka mbalimbali za Serikali baada ya maamuzi kutolewa na Mahakama. Katika kipindi cha mwaka 2020 jumla ya kilo 119.07 za heroin, kilo 3.93 za cocaine na kilo 120 za bangiziliteketezwa kwenye kiwanda cha saruji cha Twiga kilichopo Wazo Hill, Jijini Dar es Salaam.





***Kielelezo Na. 8:*** *Uteketezaji wa dawa za kulevya aina ya heroin na bangi baada ya taratibu za Kisheria kukamilika*

Juhudi za udhibiti na mapambano dhidi ya dawa za kulevya katika mwaka 2020 zilifanikisha kufunguliwa jumla ya kesi 6,877 katika Mahakama

mbalimbali Nchini. Jumla ya kesi 321 zilitolewa maamuzi mahakamani na kati ya hizo Jamhuri ilishinda kesi 218.Idadi ya kesi zilizofikishwa mahakamani kulingana na makundi na aina ya dawa za kulevya zimeainishwa katika jedwali lifuatalo;

**Jedwali Na. 7: Kesi Zilizofikishwa Mahakamani Mwaka 2020**

| Kundi la dawa | Aina ya Dawa | Kesi zilizoripotiwa | Kesi zilizofikishwa Mahakamani |
|---|---|---|---|
| Dawa za kulevya za viwandani | Heroin | 71 | 71 |
| | Cocaine | 357 | 353 |
| | **Jumla** | **428** | **424** |
| Dawa za kulevya za mashambani | Bangi | 5,902 | 5,820 |
| | Mirungi | 1,031 | 633 |
| | **Jumla** | **6,933** | **6,453** |

# SURA YA NNE

# KUPUNGUZA UHITAJI WA DAWA ZA KULEVYA

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inafafanua mkakati wa kupunguza uhitaji wa dawa za kulevya Nchini. Juhumu la msingi katika mkakati huu ni kutoa elimu kwa jamii ili ijiepushe na matumizi na biashara ya dawa za kulevya.

## 4.2 Matumizi ya Dawa za Kulevya Nchini

Dawa za kulevya zinazotumika Nchini Tanzania ni bangi, heroin, mirungi, cocaine, dawa tiba zenye asili ya kulevya pamoja na viyeyushi kama vile petroli na gundi. Hata hivyo, bangi imekuwa na idadi kubwa ya watumiaji ingawa bado kuna changamoto ya upatikanaji wa takwimu halisi ya watumiaji. Dawa inayofuata kwa matumizi ni heroin ambapo mwaka 2014 majumuisho ya tafiti mbalimbali yalikadiria kuwa kati ya watu 250,000 hadi 500,000 walikuwa wanatumia dawa hiyo na kati yao 30,000 wakitumia kwa njia ya kujidunga. Mirungi ni dawa ya tatu na cocaine ni dawa ya nne kwa matumizi Nchini.

Tatizo la dawa za kulevya limeonekana kuwa kubwa katika maeneo ya ukanda wa pwani na miji mikubwa kama vile Dar es salaam, Arusha, Mwanza, Tanga, Pwani, Morogoro, Dodoma na Mbeya. Kuna viashiria kuwa matumizi ya dawa za kulevya yamepungua nchini kutokana naidadi kubwa ya watumiaji kutafuta matibabu.

## 4.3 Sababu Zinazochangia Matumizi ya Dawa za Kulevya

Tanzania kama ilivyo katika maeneo mengine Duniani, matumizi ya dawa za kulevya yameendelea kuleta changamoto katika jamii pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali katika kukabiliana na changamoto hizo. Sababu mbalimbali zinazochangia watu kujiingiza kwenye matumizi ya dawa za kulevya kama ifuatavyo:-

i. Kukosekana kwa elimu ya kujitambua (stadi za maisha) miongoni mwa vijana. Hali hii huwasababishia kujiingia kwenye matumizi ya dawa za kulevya kwa sababu ya kukosa uwezo wa kutambua changamoto zao na njia sahihi za kutatua changamoto hizo.

ii. Kutokuwa na ufahamu mzuri juu ya madhara yanayosababishwa na matumizi ya dawa za kulevya kiafya, kijamii na kiuchumi. Asilimia kubwa ya watu wanajiingiza kwenye matumizi ya dawa za kulevya kwa lengo la kupata starehe, kujaribu kutafuta furaha, kuwa karibu na marafiki au kupunguza makali ya maisha bila kufahamu madhara wanayoweza kuyapata.

iii. Utandawazi na matumizi ya mitandao ya kijamii imekuwa kichocheo cha jamii na hasa vijana kujiingiza kwenye matumizi ya dawa za kulevya.

iv. Imani potofu, mila na desturi za baadhi ya jamii zimekuwa zikichangia matumizi ya dawa za kulevya nchini.

v. Migogoro na utengano wa kifamilia imekuwa ikisababisha kukosekana kwa malezi bora kwa watoto na vijana hali inayosababisha kukosekana kwa uangalizi wa karibu na hivyo baadhi yao kujiunga na makundi yanayotumia dawa za kulevya.

vi. Wazazi wenye uraibu wa dawa za kulevya wana uwezekano mkubwa wa kupata mtoto mwenye tatizo hilo (urithi).

vii. Mgonjwa anayetibiwa na dawa tiba zenye asili ya kulevya anapoamua kuzitumia bila kufuata maagizo ya daktari

## 4.4 Madhara ya Dawa za Kulevya

Matumizi na biashara ya dawa za kulevya husababisha madhara ya kiafya, kijamii, kiuchumi, kisiasa na kimazingira.

### Kiafya

Matumizi ya dawa za kulevya husababisha magonjwa mbalimbali yakiwemo uraibu, magonjwa ya akili, moyo, ini, kifua kikuunamagonjwa ya ngono. Matumizi ya dawa hizo kwa njia ya kujidunga huchangia kuenea kwa maambukizi ya Virusi vya UKIMWI na virusi vya homa ya ini aina B na C. Aidha, matumizi hayo yanaweza kufanya mishipa ya damu kusinyaa na inapotokea hali hiyo kwenye ubongo husababisha shinikizo la damu na kiharusi. Pia, dawa za kulevya hupunguza kumbukumbu, uwezo wa kufikiri na kufanya maamuzi sahihi. Matumizi ya kiwango kikubwa cha dawa za

kulevya kuliko alichozoea mtumiaji, husababisha vifo vya ghafla hasa kwa wajidunga.

Wanawake wajawazito wanapotumia dawa za kulevya huweza kuharibu mimba, kuzaa watoto wenye uraibu wa dawa za kulevya, watoto waliodumaa kimwili na kiakili au kujifungua watoto njiti. Madhara mengine ya kiafya ni pamoja na saratani, upungufu wa nguvu za kiume, sonona, kukosa usingizi, kukosa hamu ya kula na kuoza meno. Vilevile, matumizi ya dawa za kulevya husababisha upungufu wa kinga ya mwili dhidi ya maradhi, vidonda kwenye mfumo wa chakula kama vile vidonda vya tumbo na mara nyingine vifo. Kwa ujumla matumizi ya dawa hizi hupunguza umri wa kuishi wa mtumiaji kutokana na maradhi, uhalifu au kuzidisha kiasi cha dawa.

**Kijamii**

Matumizi ya dawa za kulevya husababisha kukithiri kwa vitendo vya kihalifu katika jamii kama wizi, ukahaba, utapeli na uporaji ambavyo hufanyika ili kupata fedha za kununulia dawa hizo. Wafanyabiashara wa dawa za kulevya huendesha magenge ya utekaji, mapigano na mauaji ili kulinda biashara zao na kuifanya jamii kuishi kwa woga. Wauzaji wa dawa za kulevya wana kawaida ya kujihusisha na biashara nyingine haramu kama vile usafirishaji wa binadamu, uuzaji haramu wa silaha, uuzaji na usafirishaji nyara za serikali, uhalifu wa kimtandao, utakatishaji fedha na ugaidi.

Matumizi ya dawa za kulevya huchangia mahusiano katika familia kuvurugika ambapo ndoa huvunjika na watoto kutelekezwa na iwapo mtoto ni mtumiaji huacha au hufukuzwa shule, hufukuzwa nyumbani na kuishi kwenye magheto ambako hubobea kwenye matumizi ya dawa za kulevya na uhalifu. Kuongezeka kwa kiasi cha maambukizi ya VVU, homa ya ini na kifua kikuu katika jamii kutoka kwa watumiaji ambao huwa na kiwango kikubwa cha maambukizi ya maradhi hayo. Unyanyapaa kwa watumiaji husababisha kukosekana haki zao za kifamilia na kijamii na hata pale wanapoacha matumizi ya dawa za kulevya familia zao au waajiri hushindwa kuwakubali. Pia, matumizi ya dawa za kulevya husababisha ajali zinazoweza kuzuilika ambazo husababisha ulemavu, vifo na uharibifu wa mali na miundombinu.

**Kiuchumi**

Matumizi ya dawa za kulevya hupunguza ufanisi kazini na huweza kusababisha kupoteza ajira au kufilisika. Mtumiaji ambaye hajapata ajira hushindwa kuajirika hivyo kusababisha umaskini kwake, jamii yake na Taifa kwa ujumla. Aidha, watumiaji wa dawa za kulevya hushindwa kujishughulisha na shughuli yoyote ile ya uzalishaji mali hivyo matumizi ya dawa hizo hupoteza nguvu kazi ya Taifa.

Mzunguko wa fedha zinazotokana na biashara ya dawa za kulevya husababisha mfumuko wa bei katika jamii na kuondoa usawa katika ushindani wa kibiashara. Biashara ya dawa za kulevya huenda sambamba na utakatishaji wa fedha ambapo madhara yake ni pamoja na kuhamisha nguvu ya kifedha kutoka kwenye Serikali, masoko na wananchi na kwenda kwa wahalifu ambao ni wafanyabiashara wa dawa za kulevya. Vilevile, utakatishaji fedha huathiri taasisi za kifedha kama vile benki pale mhalifu anapoamua kutoa fedha zake kwa mkupuo ambapo mara nyingi huwa ni kiasi kikubwa na hivyo kuiacha taasisi ya kifedha ikiyumba na kuzorotesha ukuaji wa uchumi.Tatizo la dawa za kulevya huhitaji fedha nyingi kukabiliana nalo hivyo husababisha Taifa kurudi nyuma katika jitihada za kukuza uchumi.

**Kisiasa**

Wafanyabiashara wa dawa za kulevya wanaweza kufadhili chaguzi, kuingia madarakani au kuwaondoa viongozi waliochaguliwa kidemokrasia na kuwaweka vibaraka wao ili kulinda maslahi yao. Hali hii inaweza kuathiri mustakabali wa nchi kwa kutawaliwa na magenge ya wafanyabiashara wa dawa za kulevya na jamii ya waraibu wa dawa hizo.

**Kimazingira**

Tatizo la dawa za kulevya husababisha athari za kimazingira kwa kutupwa ovyo vifaa vya kujidungia katika maeneo yasiyo rasmi mfano vichochoroni, viwanja vya michezo, fukwe na vituo vya daladala na kuiweka jamii kwenye hatari ya kupata maambukizi ya magonjwa mbalimbali. Kadhalika, wahalifu wanaolima bangi na mirungi wamekuwa wakiharibu uoto wa asili kwa kulima kwenye vyanzo vya maji hivyo kusababisha ukame, mmomonyoko wa ardhi na kutoweka kwa baadhi ya viumbe hai. Vilevile, wavutaji wa dawa za

kulevya hudhuru afya za watu walio karibu yao kwa moshi unatokana na uvutaji wa dawa hizo.

## 4.5 Jitihada Zilizofanyika Katika Kupunguza Uhitaji

Wadau wameendelea kutoa elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya katika makundi mbalimbali ya kijamii kwa kupitia vyombo vya habari, mitandao ya kijamii, tovuti za taasisi, machapisho, maadhimisho ya kitaifa, sanaa na wasanii, klabu za kupinga dawa za kulevya, semina na makongamano.

### 4.5.1 Uelimishaji Uliofanywa na Mamlaka

Mamlaka ilifanya uelimishaji katika shule za sekondari na vyuo kwenye mikoa mbalimbali. Pia ilifanya uelimishaji kwa vyombo vya ulinzi na usalama katika kanda tofauti ambazo ni Kanda ya Ziwa, Kusini, Kaskazini na Nyanda za Juu Kusini.  Halikadhalika, Mamlaka ilifanya uelimishaji kwa watumishi wa Wakala wa Huduma za Misitu Nchini (TFS) kwa lengo la kukuza ushirikiano na kufanya operesheni za pamoja ili kutokomeza kilimo cha bangi na mirungi kwenye misitu. Elimu pia ilitolewa katika maeneo mkakati ambayo ni mipaka ya Tunduma, Kasumulu, namanga, Tarakea, Holili, Manyovu, Mabamba, Mtambaswala.

Mamlaka ilifanya uelimishaji kwa umma kwenye Maadhimisho ya Siku ya kupiga vita dawa za kulevya Duniani. Uelimishaji huo ulifanyika kupitia njia ya redio, machapisho, sanaa na wasanii, runinga, mitandao ya kijamii na tovuti ya Mamlaka. Elimu pia ilitolewa katika maadhimisho ya kitaifa ya Nanenane mkoa wa Simiyu na maadhimisho ya siku ya UKIMWI Duniani mkoani Kilimanjaro.

Mamlaka ilitoa Elimu juu ya masuala ya udhibiti wa kemikali bashirifu kwa wadau 920 wakiwemo madereva wa malori ya kubeba kemikali (**187**), wasimamizi wa shughuli zinazohusu kemikali na wakaguzi (**109**), wajasiriamali wanaotumia kemikali (**520)**, maafisa biashara (**71**) na maafisa wa serikali (**33**). Uelimishaji huo ulifanyika katika vituo mbalimbali vya vya forodha.




***Kielelezo Na. 9:*** *Kamishna Jenerali, James Kaji akitoa maelezo kwa Mgeni Rasmi, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa alipotembelea banda la Mamlaka siku ya kilele cha Maadhimisho ya Nanenane, mjini Bariadi Mkoani Simiyu, mwaka 2020*

### 4.5.2 Uelimishaji uliofanywa na Wadau

Wadau mbalimbali hushiriki kutoa elimu ya dawa za kulevya ili kuhakikisha jamii kubwa zaidi inafikiwa na elimu hiyo. Serikali kupitia Mamlaka inawajibika kuratibu na kuwezesha utekelezaji wa jitihada hizo. Mwaka 2020 Asasi za kiraia zifuatazo zilitoa elimu ya dawa za kulevya kwenye jamii.

**Jedwali Na. 8: Asasi zilizotoa Elimu ya Dawa za Kulevya mwaka 2020**

| Na. | Asasi | Mkoa |
|---|---|---|
| 1 | Blue Cross Tanzania | Arusha |
| 2 | Youth Volunteers Against Risk Behaviors (YOVARIBE) | Dodoma |
| 3 | Methadone Family Against Drug Abuse (MEFADA) | Pwani |
| 4 | Organization of Youth Against Risk Behaviors (OYARB) | |
| 5 | Organization of Youth Against Risk Behaviors (OYARB) | Tanga |
| 6 | Gift of Hope Foundation | |
| 7 | Drug Abuse Fighting and Counseling Organization (DAFCO) | Mwanza |
| 8 | Youth Volunteers Against Risk Behaviors (YOVARIBE) | |
| 9 | Kirumba Movement for Harm Reduction | |
| 10 | Kikundi cha Huduma Majumbani Mbeya(Kihumbe) | Mbeya |
| 11 | Serve Tanzania (SETA) | |
| 12 | Changamoto ni Matumaini | Dar es Salaam |
| 13 | Harakati Network Organization | |
| 14 | Kibao Salama Foundation | |
| 15 | Kimara Peer Educators And Health Promoters Trust Fund | |
| 16 | Peer to Peer Supporting Group | |
| 17 | Youth Achievement Village In Tanzania (YAVT) | |
| 18 | Youth Community Rehabilitation | |
| 19 | Youth Empowerment and Psychotherapy Aid Organization | |
| 20 | Community Peers for Health and Environment Organisation (CPHEO) | |
| 21 | Tandika Youth and Handcraft Group (TAYOHAG) | |
| 22 | Methadone Family Against Drug Abuse (MEFADA) | |
| 23 | Youth Volunteers Against Risk Behaviors (YOVARIBE) | |
| 24 | International Organization of Good Templars ( T- IOGT) | |
| 25 | Kibwena Community Development | |
| 26 | Nurget Development Tanzania | |

# SURA YA TANO

# KUPUNGUZA MADHARA YA MATUMIZI YA DAWA ZA KULEVYA

## 5.1 Utangulizi

Sura hii imejikita katika kufafanua mkakati wa kupunguza madhara yanayosababishwa na matumizi ya dawa za kulevya.

## 5.2 Huduma za Upunguzaji Madhara kwa Waraibu

Serikali imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kupunguza madhara kwa kutoa tiba, huduma za utengamao na elimu ya upunguzaji madhara kwa waraibu wa dawa za kulevya. Huduma hizo ni pamoja na kupanua na kuimarisha huduma za tiba katika vitengo mbalimbali vya afya ya akili, tiba ya methadone, nyumba za upataji nafuu na huduma za unasihi. Aidha, mafunzo ya stadi za kazi yamekuwa yakifanyika kwa waraibu wa dawa za kulevya ili kuwajengea uwezo wa kujitegema na kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali. Vilevile, Mamlaka imekuwa ikiandaa miongozo mbalimbali ya kuratibu uanzishwaji na uendeshwaji wa vituo vya kutolea huduma ya methadone, usimamizi wa nyumba za upataji nafuu, uendeshaji wa vituo vya kutolea huduma za afya, asasi za kiraia na vikundi mbalimbali vinavyojihusisha na mapambano dhidi ya dawa za kulevya nchini.

### 5.2.1 Tiba ya Uraibu wa Dawa za Kulevya Katika Vitengo vya Afya ya Akili Nchini

Serikali imeendelea kusimamia na kuboresha utoaji wa tiba kwa waraibu wa dawa za kulevya katika vitengo vya afya ya akili vilivyo katika hospitali mbalimbali Nchini. Kwa kipindi cha mwaka 2020, jumla ya waraibu 169,269 ambapo wanaume ni 137,300 na wanawake ni 31,969 walipatiwa huduma ya tiba ya uraibu katika vitengo vya afya ya akili vilivyomo hospitali mbalimbali Nchini. Idadi kubwa ya waraibu walionekana kuathirika zaidi na matumizi ya vilevi kama vile pombe, bangi, mirungi, heroin na cocaine. Aidha, baadhi yao walibainika kutumia dawa za hospitali zenye asili ya kulevya kama vile valium, pethidine na tramadol kutokana na kukosekana na kupanda kwa gharama za dawa za kulevya mitaani pamoja na kuimarika kwa udhibiti wa dawa hizo.

**Jedwali Na. 9: Idadi ya Waraibu Waliopata Tiba kwenye Vitengo vya Afya ya Akili Nchini**

| Mkoa | Wanaume | Wanawake | Jumla |
|---|---|---|---|
| Temeke | 13,456 | 1,662 | 15,118 |
| Kinondoni | 15,056 | 2,651 | 17,707 |
| Ilala | 17,211 | 2,317 | 19,528 |
| Pwani | 5,643 | 1,900 | 7,543 |
| Morogoro | 4,975 | 503 | 5,478 |
| Tanga | 3,989 | 1,906 | 5,895 |
| Lindi | 4,034 | 544 | 4,578 |
| Mtwara | 5,467 | 1,322 | 6,789 |
| Ruvuma | 874 | 740 | 1,614 |
| Katavi | 613 | 371 | 984 |
| Rukwa | 578 | 333 | 911 |
| Mbeya | 6,435 | 2,034 | 8,469 |
| Iringa | 5,432 | 1,141 | 6,573 |
| Njombe | 520 | 260 | 780 |
| Kigoma | 4,000 | 1,642 | 5,642 |
| Tabora | 2,012 | 335 | 2,347 |
| Songwe | 5,987 | 1,359 | 7,346 |
| Mwanza | 10,001 | 2,264 | 12,265 |
| Kagera | 3,325 | 133 | 3,458 |
| Mara | 3,021 | 990 | 4,011 |
| Geita | 2,578 | 645 | 3,223 |
| Shinyanga | 2,456 | 789 | 3,245 |
| Singida | 1,704 | 670 | 2,374 |
| Manyara | 342 | 109 | 451 |
| Kilimanjaro | 651 | 272 | 923 |
| Arusha | 10,057 | 2,659 | 12,716 |
| Dodoma | 6,432 | 2,302 | 8,734 |
| Simiyu | 451 | 116 | 567 |
| **Jumla kuu** | **137,300** | **31,969** | **169,269** |

### 5.2.2 Huduma ya Upataji Nafuu kwenye Asasi za Kiraia

Serikali imeendelea kushirikiana na asasi za kiraia zilizosajiliwa kutoa huduma kwa waathirika wa dawa za kulevya katika jamii. Huduma zinazotolewa na asasi hizi ni pamoja na elimu, utengamao, upunguzaji wa madhara ya matumizi ya dawa za kulevya. Aidha, huduma zingine ni pamoja

na utoaji wa rufaa mbalimbali kwenda katika vituo vya afya ikiwemo kwenda katika vitengo vya afya ya akili, tiba ya methadone, nyumba za upataji nafuu na huduma zingine za utengamao.

### 5.2.3 Huduma ya Tiba Dawa

Uraibu wa dawa za kulevya unatibika kwa kutumia na dawa za hospitalini pamoja na usaidizi wa ushauri nasaha unaojulikana kitaalamu kama Medically Assisted Therapy (MAT). Mseto huu wa dawa na ushauri nasaha ni huduma iliyothibitishwa kisayansi na imeonekana kuleta tija zaidi katika tiba na kuleta mabadiliko chanya katika upataji nafuu na miongoni mwa waraibu. Tafiti za kisayansi zinaonesha mraibu anayepata mseto wa huduma ya tiba kwa kutumia dawa na unasihi anakuwa kwenye nafasi ya kupata nafuu mapema zaidi kuliko yule anayetumia dawa bila unasihi au unasihi bila dawa. Dawa zinazotumika kutibu waraibu wa afyuni kwa sasa ni Methadone, Buprenorphine na Naltrexone ingawa kwa sasa Nchini dawa zinazotumika ni Methadone na Buprenorphine.

**Methadone**

Huduma ya tiba ya methadone na usaidizi wa ushauri nasaha kwa waraibu wa dawa za kulevya ilianza rasmi mwaka 2011 ambapo Nchi yetu ilikuwa ni ya kwanza kutoa huduma hiyo upande wa bara Kusini mwa Jangwa la Sahara. Vilevile, huduma hii huhusisha wa utoaji wa tiba za magonjwa yanayoambatana na matumizi ya dawa za kulevya kama vile magonjwa ya akili, UKIMWI, kifua kikuu, magonjwa ya ngono na homa ya ini. Aidha, vituo hivyo vimekuwa vikitoa huduma zingine kama vile uzazi wa mpango, tiba kwa watoto waliozaliwa na tatizo la uraibu kutoka kwa mama zao, tatizo la udumavu pamoja na magonjwa ya kinywa, ngozi, vidonda na majipu.

Utaratibu wa utoaji huduma huanza kwa asasi za kiraia kuwaibua na kuwaandaa waraibu katika ngazi ya jamii ambapo waraibu hupata elimu sahihi na huduma ya unasihi kabla ya kufikishwa katika vituo vya tiba ya methadone. Hadi kufikia mwezi Desemba 2020, huduma ya tiba ya methadone ilipatikana kwenye vituo vya afya tisa ambapo imekuwa ikitolewa bila malipo. Vituo hivyo ni vipo katika mikoa ya Dar es Salaam (Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, hospitali za rufaa za mikoa za Temeke na

Mwananyamala), hospitali ya rufaa ya kanda ya nyanda za juu kusini-Mbeya, hospitali ya rufaa ya mkoa ya Sekou Toure-Mwanza, kituo cha Itega jijini Dodoma, hospitali ya wilaya ya Bagamoyo na hospitali ya rufaa ya Tumbi za mkoani Pwani na katika hospitali ya rufaa ya mkoa ya Bombo mkoani Tanga. Waraibu wapatao 9,188 walipatiwa huduma ya tiba ya Methadone, unasihi na tiba nyinginezo kulingana na uhitaji katika kipindi husika.

Serikali inaendelea kuongeza nguvu katika eneo hili la tiba ya Methadone na unasihi kwa kujenga vituo vingine zaidi Nchini kulingana na uhitaji na uwezo uliopo. Hadi mwisho wa mwaka 2020, vituo vitano vipya vilikuwa katika hatua ya mwisho ya ujenzi kwa ajili ya kuanza kutoa huduma mapema mwaka 2021 katika mikoa ya Arusha na Dar es Salaam (Kinondoni, Kigamboni, Temeke na Hospitali ya gereza la Segerea).

Idadi ya waraibu waliopata huduma ya Methadone tangu mwaka 2011 hadi 2020 ni 9,188 wakiwemo wanaume 8,680 na wanawake 508. Aidha, waraibu waliokutwa na maambukizi ya VVU ni 932 kati yao wanaume 732 na wanawake 200. Vilevile, waraibu waliokutwa na ugonjwa wa kifua kikuu ni 550, wanaume 504 na wanawake 46.

Tafiti zilizofanyika mwaka 2014 zinaonesha maambukizi ya VVU kwa waraibu waliokuwa wanapata tiba kwenye vituo vya methadone ni asilimia 36 ambapo yameshuka hadi asilimia 10 kufikia mwaka 2020. Hatahivyo, tafiti zinaonesha maambukizi ya VVU kwenye jamii ni asilimia 4.7 hii inaonesha maambukizi ya VVU kwa waraibu ni zaidi ya mbili ya yanayopatikana kwenye jamii hali inayoendelea kuleta changamoto kwenye jitihada za kukabiliana na janga hilo kwa waraibu.

**Jedwali Na. 10: Waraibu Waliohudumiwa na Kupewa Rufaa ya Methadone na Asasi za Kiraia, Januari hadi Desemba, 2020**

| Na. | Asasi | Mkoa | Waraibu waliohudumiwa | | | Waraibu waliopewa rufaa | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Jinsi | | | Wasiojidunga | | | Wajidunga | |
| | | | Me | Ke | Jumla | Me | Ke | Jumla | Me | Ke |
| 1. | MEFADA | Dar es Salaam | 814 | 28 | 842 | 150 | 8 | 158 | 135 | 2 |
| 2. | MEFADA | Dodoma | 855 | 7 | 862 | 53 | 1 | 54 | 1 | 0 |
| 3. | MEFADA | Bagamoyo- Pwani | 325 | 2 | 327 | 119 | 2 | 121 | 5 | 0 |
| 4. | YCR | Dodoma | 643 | 40 | 683 | 59 | 1 | 60 | 7 | 0 |
| 5. | YCR | Arusha | 239 | 7 | 246 | - | - | - | - | - |
| 6. | YCR | Bagamoyo – Pwani | 96 | - | 96 | 35 | - | 35 | 1 | 0 |
| 7. | YOVARIBE | Dar es Salaam | 2462 | 7 | 2469 | 747 | 11 | 758 | 44 | 0 |
| 8. | YOVARIBE | Dodoma | 358 | 227 | 585 | 116 | 7 | 123 | 20 | 0 |
| 9. | YOVARIBE | Mwanza | 780 | 20 | 800 | 111 | 2 | 113 | 15 | 0 |
| 10. | YOVARIBE | Tanga | 367 | 6 | 373 | 27 | - | 27 | 0 | 0 |
| 11. | Tanga Drug Free | Tanga | 170 | 152 | 18 | 46 | 5 | 51 | - | - |
| 12 | OYARB | Kibaha- Pwani | 63 | 19 | 82 | 92 | - | 92 | 2 | - |
| 13 | Organization of Youth Against Risk | Tanga | 338 | 304 | 34 | 27 | - | 27 | - | - |
| 14. | Gift of Hope Foundation | Tanga | 2168 | 236 | 2404 | 38 | 3 | 41 | - | - |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 15. | KIHUMBE | Mbeya | 115 | 2 | 117 | – | – | – | – | – |
| 16. | SETA | Mbeya | 69 | - | 69 | – | – | – | – | – |
| 17. | Tumaini | Mbeya | 43 | 1 | 44 | – | – | – | – | – |
| | **Jumla** | | **9,905** | **1,058** | **10,051** | **1,620** | **40** | **1,660** | **230** | **9,905** |



***Kielelezo Na. 10**: Kituo cha Tiba ya Methadone katika Hospitali ya Rufaa ya Mount Meru, jijini Arusha*



***Kielelezo Na. 11:** Baadhi ya Waraibu wakipata Tiba ya methadone katika hospitali ya Mount Meru Arusha.*

**Buprenorphine**

Dawa ya Buprenorphine imethibitishwa kisayansi kutibu waraibu wa afyuni kama ilivyo dawa ya methadone. Katika kipindi cha mwaka 2020, Nchi yetu imefanya majaribio ya tiba kwa waraibu 20 wa afyuni kutumia dawa ya Buprenorphine katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili. Huduma ya dawa ya Buprenorphine imekuwa ikitolewa sambamba na ushauri nasaha kwa waraibu. Dawa hii inatolewa katika mfumo wa vidonge na imeonyesha matokeo chanya katika kutibu uraibu wa afyuni. Tiba hii inatarajiwa kupanuka zaidi katika kipindi kijacho cha mwaka ili kuwafikia waraibu wengi zaidi baada ya kukamilika kwa kipindi cha majaribio.

### 5.2.4 Nyumba za Upataji Nafuu (Sober Houses)

Serikali iliendelea kuratibu uanzishwaji na kusimamia uendeshwaji wa Nyumba za Upataji Nafuu kwa kutumia Mwongozo Maalum wa Uendeshwaji wa Nyumba hizo (*Guideline Manual of Standards for Establishing and Operating Sober Houses in Mainland Tanzania*). Nyumba hizi zinaendeshwa na asasi za kiraia ambapo waraibu wa dawa za kulevya wameendelea kupata huduma kwa kupitishwa kwenye hatua 12 za upataji nafuu bila kutumia dawa ya aina yoyote. Katika kipindi cha Mwaka 2020, Nyumba 31 zilitoa huduma hiyo katika mikoa mbalimbali nchini ikiwemo Kilimanjaro, Tanga, Dar es Salaam, Pwani, Dodoma, Morogoro, Iringa, Mwanza, Kagera, Tabora na Arusha. Jedwali lifuatalo linaonesha waraibu waliopatiwa huduma kwenye Nyumba za Upataji Nafuu mwaka 2020.

**Jedwali Na. 11: Waraibu Waliopata Huduma katika Nyumba za Upataji Nafuu Mwaka 2020**

| Na. | Nyumba ya Upataji Nafuu | Mkoa | Me | Ke | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Changamoto ni Matumaini | Dar es Salaam | 31 | - | 31 |
| 2 | Changamoto ni Matumaini | Arusha | 28 | - | 28 |
| 3 | Courage on Recovery Foundation | Tanga | 64 | - | 64 |
| 4 | Drug Free Tanzania – The Right Way Recovery House | Dar es Salaam | 53 | - | 53 |
| 5 | Drug Free Tanzania – The Ties That Bind Us Recovery Center | Dar es Salaam | 44 | - | 44 |
| 6 | Gift of Hope Foundation | Tanga | 61 | - | 61 |
| 7 | Iringa Sober House | Iringa | 45 | - | 45 |
| 8 | Kilimanjaro New Vision and Sobriety | Kilimanjaro | 138 | 18 | 156 |
| 9 | Kipepeo Foundation – Free at Last Sober House | Morogoro | 64 | - | 64 |
| 10 | Kipepeo Foundation – South Beach Sober House | Dar es Salaam | 60 | - | 60 |
| 11 | Life and Hope Rehabilitation Organization | Pwani | 93 | - | 93 |
| 12 | Mrc Tanzania Kigamboni Sober House | Dar es Salaam | 292 | - | 292 |
| 13 | New Vision of Life Society Sober House (Second Chance for Addicts) | Dar es Salaam | 37 | - | 37 |
| 14 | People With Drug Dependence and Relief Foundation PEDDEREF | Dar es Salaam | 91 | 19 | 110 |
| 15 | Pillimissanah Foundation | Dar es Salaam | 191 | - | 191 |
| 16 | Pillimissanah Foundation | Mwanza | 34 | - | 34 |
| 17 | Sobriety Forever Rehabilitation Centre | Kagera | 18 | - | 18 |
| 18 | Kilimanjaro Recovery Centre | Kilimanjaro | 35 | 2 | 37 |
| 19 | Tabora Sober House | Tabora | 115 | - | 115 |
| 20 | Tanga Drug Free Organization | Tanga | 68 | - | 68 |
| 21 | Tanzania Sobriety and Rehabilitation Organization | Dodoma | 20 | - | 20 |
| 22 | Hope Again Rehabilitation and Wellness and Wellness Foundation | Dar es Salaam | 22 | 2 | 24 |
| 23 | Women's Hope Rehabilitation | Pwani | - | 15 | 15 |
| 24 | The Awaited Rehab Centre | Dar es Salaam | 19 | - | 19 |
| 25 | Mamaz and Papaz Sober house | Dar es Salaam | 78 | - | 78 |
| 26 | Foundation for Wellness and Youth Tutelage (Almotonyi Recovery House) | Arusha | 95 | - | 95 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 27 | Tanzania Sobriety Change Foundation (Arusha Recovery Sober House) | Arusha | 94 | - | 94 |
| 28 | Tanzania Sobriety Change Foundation (Meru Recovery Sober House) | Arusha | 93 | - | 93 |
| 29 | Tanzania Sobriety Change Foundation (Njiro Recovery Sober House | Arusha | 47 | - | 47 |
| 30 | Arise and Shine Sober House | Dar es Salaam | 19 | - | 19 |
| 31 | Tanzania New Future and Rehabilitation Organization | Arusha | 22 | - | 22 |
| 32 | Kilimanjaro Recovery Home | Kilimanjaro | 32 | - | 32 |
| 33 | Kilimanjaro New Vision and Sobriety | Kilimanjaro | - | 18 | 18 |
| **Jumla** | | | **2,103** | **74** | **2,177** |

## 5.3 Faida za Huduma za Upunguzaji madhara kwa Waraibu

Huduma za upunguzaji madhara kwa waraibu zinaambatana na faida mbalimbali zikiwemo: -

i. Kutibu uraibu na madhara yatokanayo na matumizi ya dawa za kulevya;
ii. Kuongeza wigo wa kupata fursa ya huduma mtambuka kwa waraibu ikiwemo tiba ya magonjwa yanayoweza kuambatana na utumiaji wa dawa za kulevya kama vile maambukizi ya VVU, kifua kikuu, homa ya ini na magonjwa ya ngono;
iii. Kuongezeka ufuasi mzuri wa dawa za kufubaza makali ya VVU na kutibu kifua Kikuu hivyo kuondoa uwezekano wa kupata usugu wa dawa hizo miongoni mwa waraibu;
iv. Kupunguza vifo vitokanavyo na kuzidisha kiwango cha matumizi ya dawa za kulevya;
v. Kuwarudisha waathirika wa matumizi ya dawa za kulevya katika shughuli za uzalishaji na hivyo kuwaondoa katika hali ya utegemezi;
vi. Kupunguza matendo ya uhalifu na uvunjifu wa Amani;

vii. Kuondoa unyanyapaa kwa wathirika wa dawa za kulevya katika jamii; na
viii. Kupungua kwa mzunguko wa fedha haramu zitokanazo na biashara ya dawa za kulevya.

# SURA YA SITA

# CHANGAMOTO NA HATUA ZA BAADAYE

## 6.1 Utangulizi

Sura hii imeainisha changamoto na hatua za baadaye katika kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya Nchini.

## 6.2 Changamoto

Zifuatazo ni changamoto zinazokabili udhibiti na mapambano dhidi ya dawa za kulevya Nchini: -

i. Ukubwa wa mipaka na ukanda mrefu wa bahari ya Hindi husababisha udhibiti wa dawa za kulevya kuwa mgumu;
ii. Kubadilika mara kwa mara kwa teknolojia inayotumika katika biashara ya dawa za kulevya;
iii. Uelewa mdogo wa jamii juu ya tatizo la dawa za kulevya;
iv. Unyanyapaa kwa waraibu wa dawa za kulevya hurudisha nyuma jitihada ya matibabu;
v. Kutokuwa na maabara ya uchunguzi ili kutafiti na kubaini dawa mpya za kulevya;
vi. Kuibuka kwa dawa mpya za kulevya (NPS) ambazo hazipo katika Sheria za Udhibiti wa Kimataifa;
vii. Kuongezeka kwa matumizi na usafirishaji haramu wa dawa tiba zenye asili ya kulevya aina ya ketamine, tramadol na tapentadol Duniani; na
viii. Waraibu kukosa shughuli za kufanya wakati wakipata huduma za methadone na nyumba za upataji nafuu na wakimaliza muda wao.

## 6.3 Hatua za Baadaye

Hatua za baadaye katika kudhibiti na kupambana na tatizo la dawa za kulevya ni kama ifuatavyo: -

i. Kuimarisha Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (Sura 95) kwa kuhuisha mara kwa mara kulingana na mabadiliko;
ii. Kupanua huduma za tiba kwa waathirika wa dawa za kulevya;

iii. Kuwajengea uwezo wadau wanaoshiriki katika udhibiti na mapambanao dhidi ya dawa za kulevya ndani na nje ya nchi; na
iv. Kuimarisha ushirikiano na mamlaka za udhibiti pamoja na wadau wote kwa ujumla.